

Hivyo ni Vipi Kuhusu Jihadi?

Moja ya mambo yaliyo kinyume ya zama hizi ni kwamba ingawa njia za mawasiliano zimeendelea kwa kiasi kikubwa mno, watu bado wana matatizo katika mawasiliano yenye maana ya makusudi kabisa na mazungumzo na tamaduni nyingine na dini mbali mbali. Kuna upotovu wa taarifa mwingi na kutoeleweka kwa imani ya Kiislam.

Watu wengi binafsi, wale wa kawaida na wataalam pia wamejaribu kuiunganisha tarehe 9/11 na dhana ya Jihadi katika Uislam. Katika moja ya mazungumzo ya maonyesho ya redio ya Toronto, mara baada ya Septemba kumi na moja, nilimsikia mpiga simu mmoja akasema kwamba kile kilichotokea siku ile kilikuwa kwa 10% ni ugaidi na 90% ni Uislam. Kiongozi mmoja wa kikristo mwenye siasa kali huko Marekani alisema katika onyesho lake la kwamba “Yumkini (inawezekana) Muhammad alikuwa gaidi.” Hivyo ni muhimu kuzungumza Kuhusu Jihadi katika Uislam.

a) Uislam ni Dini ya Amani

Uislam kimsingi ni dini ya amani. Jina lake “Islam” linatokana na neno la kiarabu “Silm” ambalo lina maana mili: moja ni “kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu” na ya pili ni “amani”. Maana zote zinaingiliana.

Wakati wowote Waislam wanapokutana, wanatumia maamkizi ya amani “as-salaam alaykum – amani iwe juu yako,” na huyo mtu mwingine anajibu kwa kusema “alaykums-salaam – juu yako iwe amani.”

ISLAM

SILM

1. Kujisalimisha kwa Allah
2. amani (kwa wanadamu wenzio)

Sala za kila siku zinaanza na kumsifu Allah kama “Rehema na Mwenye fadhila” na zinaishia na salam za amani kwa wote.

b) Dhana ya Jihad

Dhana ya Jihadi inahitaji kueleweka vizuri. Watu wengi katika vyombo vya habari wanayachukulia maneno ya Qur'ani nje ya muktadha wake. Na kwa hiyo hebu tuone ni nini maana ya Jihadi?

Hili neno "Jihad" halina maana ya "vita takatifu." Huu ni utoaji wa ki-magharibi wa dhana pana katika mafundisho ya Kiislam. Muulize mtaalam yoyote yule wa lugha ya kiarabu na atakwambia kwamba "Jihad" haina maana ya "vita takatifu." Maneno, au usemi huu wa "vita takatifu" umekuja kutokana na dhana ya Kikristo ya "vita ya haki," na umetumika hovy hovy kama lahaja ya Kiislam tangu zile siku za Krusedi.

Hivyo basi, Jihadi ina maana gani?

Katika lugha ya kiarabu, neno Jihadi kwa maana halisi ni kujitahidi na kufanya kazi kwa bidii sana kwenye jambo fulani. Katika Istitihi za Kiislam, linabakia na maana halisi hizo katika vipimo viwili tofauti, ambavyo vinaelezwa kwa "Jihadi kubwa" na "Jihadi ndogo."

Jihadi kubwa – inajulikana kama mashindano ya kiroho, mashindano kati ya nguvu mbili ndani yetu: nafsi na mwili. Moyo unapambana na matamano ya kimwili. Mapambano haya ya kiroho ni Jihadi inyoendelea ndani ya kila mmoja wetu. Uislam unawatarajia wafuasi wake kutoa kipaumbele kwenye nafsi na dhamira juu ya mwili na tamaa zake.

Kule kufunga katika mwezi wa Ramadhani ni mfano wa mafunzo ya kila mwaka kwa ajili ya Jihadi hii.

Jihadi ndogo ni yale mapambano ya silaha. Hata hivyo, hii haina maana ya moja kwa moja kwamba ni matumizi ya kufanya vurugu za kidhalimu zisizo na haki. Hii Jihadi ndogo inaweza kugawanywa kwa namna mbili: Uchokozi na ulinzi. Uchokozi na uvamizi dhidi ya watu wowote wale hauruhusiwi katika Uislam; kwa hali yoyote ile, ulinzi ni haki kamili ya kila mtu na kila Taifa.

JIHĀD

(Mapambano)

KUBWA NDOGO

(ya kiroho) (Mapambano ya silaha)

Ulinzi Uchokozi

☞ ☞

Uislam umeruhusu hii Jihad ndogo kwa ajili tu ya kuwalinda Waislam na ardhi zao, na kudumisha amani katika jumuiya za Kiislam.

Source URL:

<https://www.al-islam.org/sw/amani-na-jihadi-katika-uislam-sayyid-muhammad-rizvi/hivyo-ni-vipi-kuh-usu-jihadi>